



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilihimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika kidogo. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuendelea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu hasa yale yaliyopo nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria, kanda ya magharibi, kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine uwepo wa Kimbunga "JUDE" katika rasi ya Msumbiji, ulitawala mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kusini magharibi, kusini na maeneo jirani na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MACHI, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi ya nchi. Halikadharika mvua kubwa ziliripotiwa katika maeneo machache ya pwani ya kusini, nyanda za juu Kaskazini mashariki, ukanda wa Ziwa Viktoria, maeneo ya kati na magharibi mwa nchi. Vilevile vipindi vya upepo mkali viliripotiwa katika ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi hususani katika nusu ya kwanza ya dekada.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi, kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani, hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 MACHI, 2025

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):

Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua kubwa zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz